# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI

MKOA WA MBEYA
**Simu ya Mdomo:** 252957440/252957447
Fax: 025-2590089/2590108
Baruazoteziandikwekwa
MkurugenziMtendaji (W) Mbarali

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P 237,
**RUJEWA**.

## MAJUKUMU YA KITENGO CHA UCHAGUZI

1) Kuratibu shughuli zote zihusuzo uchaguzi (uchaguzi wa serikali za mitaa, uchaguzi mkuu na chaguzi ndogo zote zitakazo jitokeza baada ya uchaguzi kufanyika).
2) Kuratibu mazoezi yote ya uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa uchaguzi mkuu na Orodha ya wapiga kura kwa Uchaguzi wa serikali za mitaa
3) Kuratibu maswala yote muhim kwa ajili ya kuwezesha mazoez ya uchaguzi (maswala hayo ni pamoja na maandaliz ya uteuzi wa wagombea, kuratibu kampeni za wagombea, maadalizi ya vituo vya kupigia kura, mafunzo kwa washiriki wote wa uchaguzi. Mambo yote haya yanafanyika kwa ushiriji wa karibu na TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI na Wizara inayosimamia Uchaguzi wa serikali za Mitaa).
4) Kuratibu na kusimamia zoezi na uandaaji wa vituo vya kuandikishia wapiga kura na Vituo vya kupigia kura
5) Kuratibu na kusimamia zoezi zima la upigaji kura katika chaguzi zote katika eneo la Halmashauri
6) Kutunza kumbukumbu mbalimbali za Uchaguzi
7) Kushirikiana na Idara ya Utumishi kuhakikisha mafunzo ya mara kwa mara yanafanyika kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa Mujibu wa Sheria
8) Kumshauri Mkurugenzi juu ya maswala yote yahusuyo uchaguzi katika Halmashauri ili kuwezesha mazoezi hayo kufanyika kwa mujibu wa Sheria
9) Kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu zoezi la uandikishaji na upigaji kura
10) Kutekeleza majukumu mengineyo kwa maelekezo ya Mkurugenzi wa Halmashauri